# TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA TATU WA MWAKA

## DCB Commercial Bank Plc

Taarifa inatolewa kwamba, Mkutano Mkuu wa Ishirini na Tatu wa mwaka wa Benki ya DCB, utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 19 Julai 2025 kwa njia ya mtandao (Zoom Conference), kuanzia saa nne kamili (4:00) asubuhi.

**AGENDA**

1. Kufungua mkutano mkuu wa mwaka
2. Kuridhia agenda ya Mkutano Mkuu wa Ishirini na tatu wa mwaka
3. Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa 22 wa mwaka uliofanyika tarehe 14 Septemba 2024
4. Kupokea na kuridhia utekelezaji wa yatokanayo na Mkutano Mkuu wa 22 wa mwaka
5. Kupokea na kuridhia
   - 5.1 Taarifa ya wakurugenzi ya mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba, 2024
   - 5.2 Taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba, 2024
   - 5.3 Taarifa ya mkaguzi huru ya hesabu zilizokaguliwa za mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba, 2024
6. Kupokea na kuridhia Mabadiliko ya Vifungu vya Katiba ya Kampuni
7. Kuridhia uteuzi wa wajumbe wa Bodi
8. Kuteua mkaguzi huru wa hesabu kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Disemba 2025
9. Kupokea na kuridhia pendekezo la malipo ya ada kwa wajumbe wa bodi
10. Kupanga tarehe ya Mkutano Mkuu wa ishirini na nne
11. Mengineyo
12. Kufunga mkutano

**MAELEZO**

1. Wanahisa wanaotarajia kuhudhuria mkutano mkuu wanatakiwa wawe na CDS namba ambazo zinapatikana kwenye risiti ya uwekezaji wa hisa (depository receipt) au taarifa ya akaunti (CSDR account statement).

2. Wanahisa ambao hawataweza kuhudhuria Mkutano wanaruhusiwa kuchagua wawakilishi watakaohudhuria na kupiga kura kwa niaba yao kwa kuzingatia sheria na Katiba ya Kampuni. Fomu ya uwakilishi (Proxy Form) lazima ijazwe na kuwasilishwa kwenye ofisi ya Katibu wa Benki iliyopo Makao Makuu ya DCB Magomeni Mwembechai au kwa njia ya mtandao kupitia barua pepe **shareholder@dcb.co.tz** au matawini kabla ya saa 4 asubuhi siku ya Ijumaa tarehe 18 Julai 2025.

3. Nakala za taarifa ya mwaka na fomu za mwakilishi (proxy forms) zitapatikana matawini na kwenye tovuti ya benki **(www.dcb.co.tz).**

4. Orodha (Register) ya wanahisa itafungwa siku ya Jumanne tarehe 15 Julai 2025.

5. Mapendekezo ya wanahisa yawasilishwe kwenye ofisi ya Katibu wa Benki au kwa barua pepe kabla ya saa 8 mchana siku ya Jumatano tarehe 16 Julai 2025.

**KWA IDHINI YA BODI,**

**Regina Mduma**
**Katibu wa Kampuni**
**26 Juni 2025.**